



THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL

Gredi ya 8

Septemba/ Oktoba 2026

Mwongozo wa Kutathminia

SEHEMU B na C

Mwongozo huu una kurasa 11 zilizopigwa chapa.

© KNEC 2026

ZOEZI 3: KUSOMA KWA UFAHAMU

1. Ni kivutio cha mvua
Hutupatia dawa za kiasili

Hoja 1 x1 =1

2. Hasara za kutotunza maliasili:
- i. Kukosa pesa za kigeni
 - ii. Tutapata magonjwa
 - iii. Tutakosa mvua
 - iv. Viumbe wataangamia
 - v. Nchi itakosa kupendeza

Hoja 1 x1 =1

3. Njia ya kuzuia mmonyo wa udongo:
- i. Kupanda miti
 - ii. Kupanda nyasi
 - iii. Kutolima sehemu za miteremko
 - iv. Kuchimba mitaro.
 - v. Kujenga vizuizi

Hoja 1 x1 =1

4. Maana ya kuupiga jeki
- i. Kuimarisha
 - ii. Kukuza
 - iii. Kuinua
 - iv. Kuboresha
 - v. Kusaidia kuimarisha

Hoja 1x1 =1

5. Wao ndio wanaorithishwa thamani na amali za jamii ili kuzitunza na kuzipokeza kwa vizazi vingine.

Hoja 1x1 =1

6. C.

Hoja 1x1 =1

7. Hatua za kuchukuliwa kwa wanaodhulumu watoto:
- i. Watakamatwa
 - ii. Watafungwa
 - iii. Wataonywa
 - iv. Watashauriwa

Hoja 1x1 =1

Tanbihi

Hakiki majibu ya mwanafunzi ipasavyo

Hoja 1x1 =1

8. Kosa, kinyume cha sheria, uhalifu

Hoja 1x1 =1

MIPAKA YA KUTUZIA SEHEMU (B)

UFAHAMU WA KUSOMA (READING COMPREHENSION)

UPEO/ALAMA (SCOPE)	KIWANGO CHA UTENDAJI (PERFORMANCE LEVELS)
7-8	4
5-6	3
3-4	2
1-2	1

ZOEZI 4: UFUPISHO

9. Manufaa ya mitandao

Mitandao inawawezesha watu kuwasiliana, kuendeleza biashara, kujifunza na kujipatia riziki.

(maneno 10)

Hoja 1x1= 1

10. Methali inayojumuisha ujumbe katika aya ya kwanza.

Hoja 1x1= 1

- Hakuna mchele ukosao ndume.
- Hakuna masika yasiyokuwa na mbu
- Hakuna bamvua lisilo usubi.

11. Ujumbe wa kauli zilizokolezwa rangi katika aya ya pili.

Wengine huwasababishia wenzao dhiki za kisaikolojia, kuchukua utambulisho kwa manufaa yao/kufanya uhalifu.

(Maneno 11)

Hoja 1x1= 1

12. Kukomesha uhalifu ni jukumu la mtu binafsi.

Tunafaa tutumie nywila imara kila wakati, kuepuka kusakura tovuti au viungo visivyoaminika, kutotangamana na watu tusiowafahamu na kuwaripoti washukiwa.

Hoja 1x1= 1

UFUPISHO (SUMMARY)

UPEO (SCOPE)	KIWANGO CHA UTENDAJI (PERFORMANCE LEVELS)
4	4
3	3
2	2
1	1

ZOEZI 5: MATUMIZI YA LUGHA

13. C (alama 1)
14. A (alama 1)
15. D (alama 1)
16. B (alama 1)
17. B (alama 1)
18. Vichache (alama 1)
19. Salaala! **Meli** hiyo imeng'oa nanga na mizigo hiyo yote?
Vitahiniwa vimekolezwa rangi. (alama 2/0)
20. **u na ya** (alama 2)
21. (i) Kombo hufuma fulana yake kwa uzi imara. (alama 1)
(ii) Vidizi vya vitoto vyangu vimepikwa vizuri. (alama 1)
22. Ushauri nasaha wake **uliunganisha** marafiki hao (alama 2)
23. Julita na Paulo hawajawasaidia mayatima (alama 2/0)
24. “Waimbieni/ imbieni wenzenu nyimbo mlizotunga.” Mwalimu aliwambia Talia na Jeni.
(alama 2/0)
25. Pendo alipalilia shamba lake ambalo lilikuwa na magugu tele (alama 2)

SARUFI (GRAMMAR)

UPEO (SCOPE)	KIWANGO CHA UTENDAJI (PERFORMANCE LEVELS)
16-20	4
11--15	3
6-10	2
1-5	1

ZOEZI 6 : KUANDIKA (alama 10)

26. Hii ni insha ya kubuni ya masimulizi.

i. Iwe na muundo bayana wenye

- Kichwa
- Utangulizi
- Mwili
- Hitimisho,

ii. Mwanafunzi asimulie kisa kinachomalizika na kauli aliyopewa. Izingatie matukio ya likizo.

iii. Kisa kioane na kiini cha kauli aliyopewa- ionyeshe matukio ambayo yanayomfanya mhusika kukumbuka.

iv. Matukio yatiririke kwa mfuatano ufaao; hata anapotumia mbinu rejeshi ahakikishe matukio yamehusiana vyema.

v. Ateue vipengele vifaavyo vya lugha kuwasilisha matukio. Kwa mfano tamathali za usemi kama vile nahau, sitiari na chuku.

vi. Insha izingatie sarufi na hijai sahihi.

vii. Iwe na uakifishaji ufaao.

viii. Anaweza kuchagua mtindo au nafsi moja ya usimulizi au akachanganya. Kwa mfano nafsi ya kwanza na ya tatu. Anaweza pia kuchanganya nafsi.

ix. Wahusika wawe bayana

Tanbihi:

- i. Mwanafunzi ana uhuru wa kuzingatia masuala yoyote yanayohusiana na maudhui ya insha lengwa.
- ii. Katika kutuza, mwalimu azingatie vigezo vifuatavyo ili kutathmini kiwango cha utendaji cha mwanafunzi. Viwango hivyo ni Kiwango cha 4, 3, 2 na 1
- iii. Kiwango hicho ndicho atakachorekodi kwenye jedwali la alama.

Viwango vya kutathminia

Vigezo vya kutathminia	Kuzidi matarajio 4	Kufikia matarajio 3	Kukaribia matarajio 2	Mbali na matarajio 1
Sarufi na ufundi wa uandishi	Anadhihirisha umilisi wa kiwango cha juu cha sarufi, uakifishaji na uendelezaji wa maneno katika uandishi wake.	Anatumia sarufi, alama za uakifishaji na kuendeleza maneno ipasavyo katika uandishi. Hata hivyo, ana makosa machache ambayo hayatatizi usomaji.	Ana makosa ya sarufi, uakifishaji na maendelezo ya maneno ambayo yanatatiza usomaji wa sehemu za insha yake.	Ana makosa mengi ya sarufi, uakifishaji na maendelezo ya maneno kuanzia mwanzo hadi mwisho wa uandishi. Msomaji anaweza tu kukisia maana.
Mwandiko	Ana mwandiko nadhifu unaosomeka kwa urahisi. Anatenganisha herufi zote ipasavyo kwenye mistari. Anaacha nafasi inayofaa baina ya maneno kutoka mwanzo hadi mwisho wa insha.	Ana mwandiko nadhifu unaosomeka kwa urahisi. Anatenganisha herufi nyingi ipasavyo. Anaacha nafasi inayofaa baina ya maneno.	Ana mwandiko usio nadhifu lakini unasomeka. Anatenganisha baadhi ya herufi ipasavyo. Anaacha nafasi zisizolingana baina ya maneno.	Ana mwandiko usiosomeka kwa urahisi. Hatenganishi herufi nyingi ipasavyo. Anaacha nafasi nyingi zisizolingana baina ya maneno.
Msamiati	Ana uteuzi mzuri wa maneno na matumizi anuwai ya msamiati kulingana	Ana uteuzi mzuri wa msamiati uliotumika	Anatumia msamiati finyu ambao wakati mwingi haulingani na	Anatumia msamiati finyu ambao haulingani na

	na muktadha.	kulingana na muktadha.	muktadha.	muktadha.
Mpangilio (Muundo na mtindo)	Ana uwiano na mpangilio wa kipekee wa mawazo kuanzia mwanzo hadi mwisho. Amebainisha utangulizi, mwili na hitimisho vilivyo. Anaendeleza mawazo vizuri.	Ana mtiririko wenye mantiki. Kuna uwiano na mfululizo wa mawazo. Kuna utangulizi, mwili na hitimisho. Anaendeleza mawazo vizuri.	Anajaribu kupanga mawazo kimantiki. Utangulizi, mwili na hitimisho hujitokeza kwa kiasi. Anaendeleza baadhi ya mawazo vizuri.	Hana mpangilio unaoeleweka wa mawazo na ni vigumu kufuatilia kazi yake.

KUANDIKA (WRITING)

UPEO (SCOPE)	KIWANGO CHA UTENDAJI (PERFORMANCE LEVELS)
8-10	4
5-7	3
3-4	2
1-2	1

ZOEZI 7 : FASIHI (Alama 20)

SEHEMU C

26. a. Ithibati ya kisasili
- i. Kisa kinasimulia chanzo cha jamii ya Wakamba
 - ii. kinaelezea kwa nini jamii ya Wakamba imetawanyika
 - iii. Kina misingi ya imani za kidini- Mulungu kuumba jamii ya Wakamba.

Hoja 2x1=2

b. Mafunzo

- i. Ni vyema kuwa na shukrani
- ii. Ubinafsi huleta hasara
- iii. Mkondo wa maisha ya binadamu unaweza kubadilika kwa sababu ya matendo ya binadamu mwenzake.
- iv. Maadili ya kidini- kumcha Mungu/ kutotoa kafara kulisababisha madhara

Hoja 2x1=2

c. Kufanikishwa kwa uwasilishaji

- i. hata wewe ungejiuliza hivyo hivyo
- ii. hakuwafinyanga kwa udongo... la hasha
- iii. bila shaka unaweza kukisia matokeo ya haya
- iv. naye binadamu ni nani?

Hoja 1x1=1

d. Mbinu ya kuwasilisha:

- i. nitaigiza
- ii. nitapandisha sauti
- iii. nitaashiria mbinguni kwa kidole

(alama 2)

e. Mbinu

- i. Kuhusisha hadhira
- ii. Kuishawishi hadhira ikubaliane na mtazamo wake

Hoja 1x1=1

f. Vipengele vya lugha:

(alama 2)

Nahau - kipusa wakuonewa kijicho, kupata majiko, mkono wa birika, kifunguamimba

Tashbihi- Hakuwafinyanga kwa udongo kama chungu. Vyote hivi viliwazunguka kana kwamba vinawaabudu.

Urudiaji – si mifugo, si mashamba, ikaicharaza, ikaicharaza ardhi,

Tashhisi- Ardhi yenyewe ikaanza kulalamika

Tanakali – vilivyojaa furifuri

Methali- uwahi udongo uli maji

Chuku- hata kafara ya mbuzi aliyemaa mguu walishindwa kutoa.

Uzungumzi wa moja kwa moja na hadhira

Tashihisi- Janga la njaa liliwakondolea macho.

27. TAMTHILIA

a) Sifa za tamthilia zinazojitokeza katika sehemu hii:

- i. Kuwepo kwa Sehemu na Onyesho
- ii. Kuwepo kwa maelekezo ya jukwaani
- iii. Mazungumzo baina ya wahusika.
- iv. Matukio kutokea/ kuigizwa katika mandhari maalumu

Hoja 2x1= 2

b) Maudhui yanayojitokeza:

- i. **Uwekezaji-** Kuanzisha mradi wa kufuga kuku, Rasiberi ni mfugaji
- ii. **Mahusiano ya kifamilia-** Maarifa na Pendo wanajadiliana mradi.
- iii. **Uwajibikaji-** Maarifa kuweka akiba, Pendo kuwatembelea wazazi.
- iv. **Dhiki zinazowakumba wafanyakazi.** Maarifa kustaafishwa

Hoja 3x1-3

c) Sifa za Pendo

- i. **Mwenye mlahaka mwema-** ana uhusiano mwema na mume wake.
- ii. **Mwenye kuwajibika-** anashughulikia mahitaji ya nyumbani
- iii. **Mnyenyekevu-** anamuunga mkono bwana wake
- iv. **Mshauri-**anamwelekeza mumewe kwa Rasiberi
- v. **Mwenye hekima-**anamshauri bwanake kupata ushauri kutoka kwa Bi. Rasiberi.

Hoja 3x1-3

Hakiki majibu ya mwanafunzi ipasavyo.

d) Mbinu za lugha zilizotumika katika dondoo :

- i. **Tashihisi** – Gharama ilikuwa inaelekea kunibwaga chini.
- ii. **Nahau-** akipasua kimya

Hoja 2 x 1 = 2

FASIHI (LITERATURE)

UPEO (SCOPE)	KIWANGO CHA UTENDAJI (PERFORMANCE LEVELS)
16-20	4
11-15	3
6-10	2
1-5	1



KISWAHILI GRADE 8 ASSESSMENT SHEET: SEHEMU B

(Tumia vigezo vya kutathminia ili kurekodi kiwango cha utendaji cha mwanafunzi: 4, 3, 2 ama 1)

		UFAHAMU WA KUSOMA				UFUPISHO				SARUFI				KUANDIKA				FASIHI				MAONI KUHUSU UTENDAJI
NO	JINA LA MWANAFUNZI	4	3	2	1	4	3	2	1	4	3	2	1	4	3	2	1	4	3	2	1	